# OFISI YA MKUU WA MKOA KIGOMA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KILIMO MSIMU WA 2016/2017 NA MAANDALIZI YA KILIMO MSIMU WA 2017/2018

ILIYOTOLEWA KWENYE KAMATI YA USHAURI YA MKOA (RCC)
TAREHE 13 OKTOBA 2017



# MPANGILIO

- Utangulizi.
- Utekelezaji kwa mwaka 2016/2017 na Hali ya Chakula.
- Changamoto zinazokabili usalama wa chakula.
- Mkakati wa kupambana na changamoto.
- Upatikanaji wa Pembejeo mwaka 2016/2017.
- Maandalizi ya msimu wa 2017/2018.

# Utangulizi

- Sekta ya Kilimo inatoa ajira  kwa zaidi ya 80% ya wakazi wa Mkoa wa Kigoma.

- Mkoa unakadiriwa kuwa na eneo la hekta 2,668,630 linalofaa kwa kilimo.

- Kwa sasa eneo linalotumika kwa kilimo ni takriban hekta 896,895 tu, sawa na 34% ya eneo linalofaa kwa Kilimo.

# Utekelezaji kwa mwaka 2016/2017 na Hali ya Chakula

- Katika msimu wa mwaka 2016/2017 eneo lililotengwa kwa ajili ya mazao ya chakula na biashara ni hekta 847,797:
  - **Mazao ya chakula**: hekta 756,556 zilizotarajiwa kuzalisha tani 1,700,988 za mazao mbalimbali ya chakula
  - **Mazao ya biashara**: hekta 91,241 ambazo zilitarajiwa kuzalisha tani 132,239.
- Tathmini iliyofanywa mwishoni mwa mwezi Mei 2017 ilibaini kuwa:
  - Kwa upande wa mazao ya chakula eneo lililolimwa ni hekta 632,200 na kuzalisha tani 1,506,452.80 sawa na 88% ya lengo la uzalishaji
  - Kwa upande wa mazao makuu ya biashara kwa maana ya pamba, tumbaku, kahawa na miwa, eneo lililolimwa ni hekta 27,305 na kuzalisha tani 49,162 sawa na 37% ya lengo.

# Utekelezaji

- Jedwali Na. 2 Hali ya upatikanaji Chakula Kigoma

| HALMASHAURI/WILAYA. | UZALISHAJI (TANI) | IDADI YA WATU | MAHITAJI (TANI) | ZIADA/PUNGUFU (TANI) |
|---|---|---|---|---|
| Kigoma DC | 149,534.30 | 240,528 | 54,870.45 | 94,663.85 |
| Buhigwe DC | 163,975.00 | 289,160 | 65,964.63 | 98,010.38 |
| Uvinza DC | 416,649.00 | 436,158 | 99,498.54 | 317,150.46 |
| Kasulu Dc | 358,626.00 | 484,083 | 110,431.43 | 248,194.57 |
| Kasulu TC | 137,230 | 236,751 | 54,008.82 | 83,221.18 |
| Kigoma/Ujiji MC | 17,558.90 | 244,953 | 55,879.90 | -38,321.00 |
| Kakonko DC | 121,049.65 | 190,492 | 43,455.99 | 77,593.66 |
| Kibondo DC | 141,829.95 | 297,106 | 67,777.31 | 74,052.64 |
| **JUMLA** | **1,506,452.80** | **2,419,231** | **551,887.07** | **954,565.73** |

# Changamoto katika usalama wa chakula na mikakati

Changamoto:

- Uvushaji wa chakula kiholela hususani muhogo kwenda nje ya nchi (Burundi na DRC) kwa kutumia njia zisizo rasmi
- Upungufu wa maghala kwa ajili ya kuhifadhia mazao pindi yanapovunwa.

Mikakati:

- Kuendelea kuelimisha wananchi kuhakikisha wanahifadhi chakula cha kutosha mara baada ya mavuno
- Kutotumia vibaya chakula kilichopatikana kwa msimu 2016/2017 hususani katika sherehe na kutengenezea pombe za kienyeji
- Kuhimiza maandalizi ya mashamba mapema ili mvua zinaponyesha ziwe za kupandia na siyo za kuandaa mashamba na kulima

## Mkakati wa kupambana na changamoto……………

- Angalau kila kaya kupanda eka 2 za zao la muhogo.
- Kupanda mazao ya muda mfupi (mfano, kunde, maharage, mahindi ya muda mfupi).
- Kupanda mazao yanayostahimili ukame mfano mtama, muhogo, kunde na viazi vikuu.
- Kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia maji ya mito iliyopo na kuvuna maji ya mvua.
- Kuhamasisha na kuimarisha ufugaji wa kuku, bata, samaki na nyuki ili wakulima waweze kuuza na kujinunulia chakula na kujipatia kitoweo.
- Kujenga maghala zaidi na kuboresha yaliyopo ili kuwezesha uhifadhi wa chakula cha kutosha na cha uhakika.
- Kudhibiti utoroshaji wa chakula kwenda nje ya nchi kwa kusimamia maelekezo kutoka Wizara ya Kilimo.

# Upatikanaji wa Pembejeo za Ruzuku na Changamoto, mwaka 2016/2017

## Hali ya upatikanaji:

- Msimu wa mwaka 2016/2017 Mkoa wa Kigoma ulipatiwa mgawo wa tani 900 za pembejeo ya ruzuku ambayo ni mbolea ya kukuzia mahindi na mpunga.
- Mgawanyo wa mbolea kwenye Halmashauri ni kama ilivyooneshwa kwenye jedwali Na. 2.

## Changamoto:

- Mbolea kuchelewa kuwafikia wakulima na kukuta tayari mazao yameshaota hivyo kupunguza uhitaji.
- Baadhi ya Mawakala kutokuwa na uwezo wa kusambaza pembejeo kikamilifu.
- Baadhi ya wakulima kutokuwa na fedha za kuweza kununulia pembejeo

# Upatikanaji wa Pembejeo za ruzuku na Changamoto, mwaka 2016/2017…….

- Jedwali Na. 2 linaonyesha mgawo wa pembejeo 2016/2017.

| HALMASHAURI/WILAYA | MGAO (TANI) | KIASI KILICHOTUMIKA (TANI) | KIASI KILICHOBAKI (TANI) |
|---|---|---|---|
| KIGOMA | 90 | 90 | 0 |
| UVINZA | 190 | 110.1 | 79.9 |
| BUHIGWE | 86 | 86 | 0 |
| KASULU DC | 214 | 185 | 29 |
| KASULU TC | 45 | 45 | 0 |
| KAKONKO | 90 | 90 | 0 |
| KIBONDO | 158 | 158 | 0 |
| KIGOMA/UJIJI | 27 | 27 | 0 |
| **JUMLA** | **900** | **791.1** | **108.9** |

# Maandalizi ya msimu wa Kilimo 2017/2018

- Msimu wa Kilimo Mkoa wa Kigoma tayari umeshaanza:
  - Halmashauri zote zimeshaelekezwa kuwahimiza wakulima kufanya maandalizi ya mwisho.
  - Maandalizi yote muhimu yanayotakiwa kukamilishwa ni pamoja na kusafisha mashamba ikiwa ni pamoja na kuyalima ili mvua zitakaponyesha waanze kupanda badala ya kuanza matayarisho.
- Upatikanaji wa Pembejeo za Ruzuku mwaka 2017/2018:
  - Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, imebadili utaratibu wa utoaji wa pembejeo za kilimo ambapo Kanuni za mbolea za mwaka 2011 zimefanyiwa marekebisho kupitia ***The Fertilizer (Amendment) Regulations, 2017***
  - Marekebisho hayo ya Kanuni yanaelekeza kudhibitiwa kwa bei ya mbolea na kutoa bei elekezi
  - Mamlaka ya Udhibiti wa mbolea Tanzania tayari imeshatangaza bei elekezi kwa mbolea za kupandia (DAP) na kukuzia (UREA), ambapo maelekezo ya ndani zaidi yapo kwenye mwongozo uliotolewa tarehe 7 Septemba ,2017 na Wizara ya Kilimo